JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI


# JARIDA LA MAWASILIANO


*Toleo la 25*

*#Kazilendelee*


## SEKTA YA MAWASILIANO YAZIDI KUNG'ARA

*#TanzaniayaKidijiti*



# BODI YA WAHARIRI

## Mwenyekiti

**Dkt. Jim Yonazi**

Katibu Mkuu, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

## Mhariri

Bw. Innocent Mungy

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

## Mratibu

Tagie Daisy Mwakawago

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini katika Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

## Waandishi na Maafisa Habari

Faraja Mpina
Chedaiwe Msuya
Jumaa Wange

## Msanifu na Picha

Jumaa Wange

# Sekta ya Mawasiliano yazidi Kung'ara



Dkt. Jim Yonazi
Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imezidi kung'aa kimataifa kwa kufanikisha malengo na mikakati iliyojipangia katika kukuza na kurahisisha huduma za sekta ya mawasiliano ndani na nje ya nchi. Mafanikio hayo yanaanzia nchini kufuatia Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kuzidi kuwezesha miundombinu ya mawasiliano ndani na nje ya nchi. Kilometa zaidi ya 8,000 kati ya 15,000 za Mkongo zimeshakamilika kwa kuunganisha Makao Makuu ya Wilaya 23 nchini kati ya 66 zilizopo nchini.

Aidha, mawasiliano ya intaneti ya kasi yamefikishwa katika Mlima Kilimanjaro, ambapo watalii wameanza kutuma salamu na matukio mbalimbali kwa ndugu, jamaa, marafiki na dunia kwa ujumla kwa urahisi. Kadhalika, teknolojia ya 5G imezinduliwa nchini hivi karibuni kupitia Kampuni ya simu ya Vodacom Tanzania ambapo teknolojia hiyo itakuwa na manufaa katika sekta zote za uchumi na kijamii nchini.

Vile vile, Mradi wa Anwani na Makazi umewezesha kufanikisha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lililoanza Kitaifa tarehe 23 Agosti 2022 kutokana na kurasimisha majina ya mitaa na anwani za makazi ya watu nchini.

Kwa upande wa kimataifa, hivi karibuni Tanzania imekuwa mjumbe wa Baraza la Umoja wa Mawasiliano Afrika (African Telecommunication Union – ATU), ambayo ni hatua muhimu ya kuinadi Tanzania katika sekta ya mawasiliano duniani. Aidha, Tanzania pia ni Mwakilishi wa Mabaraza Mawili ya Umoja wa Posta Duniani, yaani Mjumbe wa Baraza la Utawala na Mjumbe wa Baraza la Uendeshaji wa Posta Duniani wenye jumla ya nchi wanachama 192.

Kadhalika, Wizara imefanikiha Kongamano kubwa linalokutanisha wadau wa ndani na nje ya nchi katika sekta ya habari na mawasiliano. Kongamano hilo la Connect to Connect "C2C" lilifanyika katika Hoteli ya Serena, jijini Dar es Salaam tarehe 7 na 8 Septemba 2022, ambapo washiriki zaidi ya 350 walijadili masuala ya TEHAMA na mifumo yake, uhusishwaji wa sekta ya mawasiliano katika maendeleo Barani Afrika, kutanua wigo wa miundombinu ya TEHAMA, yakiwemo masuala ya sera, sheria na usalama wa mifumo.

Wizara pia inajipanga kushiriki katika Mkutano wa Kimataifa wa Mawasiliano ulioandaliwa na Shirika la Kimataifa la Mawasiliano (ITU) nchini Romania mwishoni mwa mwezi Septemba 2022. Tanzania inagombea nafasi ya kuwa mjumbe wa baraza la ITU.

Aidha, Wizara pia inaratibu ushiriki katika Kongamano la Biashara na Uwekezaji katika Sekta ya Mawasiliano litakalofanyika katika nchi ya Jamhuri ya Demokrasia ya Congo mwezi Oktoba 2022. Kongamano hilo linatoa nafasi ya kutangaza fursa za biashara na uwekezaji zilizopo nchini katika sekta ya mawasiliano.

Wizara itaendelea kutekeleza malengo iliyojipangia na kubuni mikakati yenye dira ya kuleta mapinduzi chanya katika sekta ya mawasiliano. Ni matarajio kuwa Watumishi wa Wizara na Taasisi zake wataendelea kujituma katika kubuni mikakati endelevu na imara zaidi, ili sekta ya mawasiliano izidi kupiga hatua za kiteknolojia na kuwa shindani katika jukwaa la kimataifa.



# TANZANIA YACHAGULIWA BARAZA LA UMOJA WA MAWASILIANO AFRIKA (ATU)

Tanzania imechaguliwa kuwa mjumbe wa Baraza la Umoja wa Mawasiliano Afrika (African Telecommunications Union - ATU) kwa kipindi cha miaka 4 (2023-2026).

Tanzania ni miongoni mwa nchi 25 zilizochaguliwa kati ya nchi wanachama wa Umoja wa Mawasiliano Afrika (ATU) 49.

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliongoza kampeni ya Tanzania kuomba nchi wanachama wa ATU kuichagua Tanzania katika uchaguzi uliofanyika kwenye Mkutano Mkuu wa sita wa Umoja huo (Conference of Plenipotentiaries) unaofanyika Jijini Algiers, Algeria.

Akichangia hoja katika Mkutano huo leo, Mheshimiwa Nape alisisitiza juu ya umuhimu wa nchi za Afrika kujipanga kimkakati hususan katika chaguzi zinazofanyika katika mashirika ya Mawasiliano ya Kimataifa ikiwemo Shirika la Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU - International Telecommunications Union). Akichangia hoja katika Mkutano huo leo, Mheshimiwa Nape alisisitiza juu ya umuhimu wa nchi za Afrika kujipanga kimkakati hususan katika chaguzi zinazofanyika katika mashirika ya Mawasiliano ya Kimataifa ikiwemo Shirika la Umoja wa Mawasiliano Duniani (ITU - International Telecommunications Union).





# TANZANIA YAFIKISHA MAWASILIANO YA INTANETI YENYE KASI MLIMA KILIMANJARO

Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL) imefikisha huduma ya mawasiliano ya intaneti yenye kasi katika Mlima Kilimanjaro.

Mlima huo mrefu zaidi barani Afrika, unaopatikana katika Mkoa wa Kilimanjaro nchini Tanzania umefikishiwa mawasiliano ya intaneti yenye kasi ili kuendelea kukuza Sekta ya utalii na upatikanaji wa huduma za kidijiti katika mlima huo.

Hayo yamezungumzwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (Mb) katika hafla ya uzinduzi wa huduma za mawasiliano ya intaneti katika Mlima huo iliyofanyika kituo cha Horombo cha Mlima Kilimanjaro, Agosti 16, 2022.

Amesema kuwa huduma ya intaneti yenye kasi imefika katika kituo cha Mandara chenye umbali wa mita 2700, Kituo cha Homboro mita 3720 na Kituo cha Kibo mita 4720 juu ya usawa wa bahari huku matarajio ni kufikisha umbali wa mita 5895 katika kilele cha Uhuru ifikapo mwezi Desemba 2022.

Waziri Nape amezungumzia ufikishaji wa huduma ya intaneti yenye kasi katika Mlima Kilimanjaro kuwa ni tukio la kihistoria kwa nchi ya Tanzania na Bara zima la Afrika kwa kufungua fursa ya watalii na waongoza utalii kufanya mawasiliano ya mubashara na ndugu na familia zao wakiwa katika mlima huo.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Nurdin Babu amesema kuwa Mhe. Rais Samia ameifungua sekta ya utalii nchini na Serikali anayoiongoza kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeweka mazingira wezeshi ya sekta ya utalii kukua zaidi kwa kufikisha huduma ya intaneti ya kasi katika Mlima Kilimanjaro.

Kwa upande wa Naibu Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Bw. Mohammed Khamis Abdulla amelipongeza Shirika la TTCL kwa kutatua moja ya changamoto ya muda mrefu ya ukosefu wa huduma za mawasiliano katika maeneo ya hifadhi na kulitaka Shirika hilo kuyafikia maeneo mengi zaidi.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Mhandisi Peter Ulanga amesema kuwa mradi huo wa kufikisha mawasiliano ya intaneti yenye kasi katika Mlima Kilimanjaro kwa gharama ya milioni 146 utekelezaji wake haukuwa rahisi lakini umewezekana kutokana na ushirikiano mkubwa walioupata kutoka katika Mamlaka ya Hifadhi ya Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA).



# TEKNOLOJIA YA 5G YAFIKA TANZANIA

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Nape Nnauye (Mb) amesema Serikali kupitia Wizara ya Habari inaunga mkono kikamilifu sekta binafsi na mfumo wa teknolojia ya uvumbuzi zinaongezwa katika kutoa suluhisho na kusaidia nchi kufikia malengo yake ya SDG.

Waziri ameyasema hayo Septemba 1 2022 katika ukumbi wa mikutano Mlimani City jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa serikali inapongeza maendeleo haya yaliyozinduliwa rasmi kibiashara hapa nchini na Upatikanaji wa mtandao wa kasi unaojulikana kama "Wireless ya Fibre" na kuipongeza Kampuni ya Vodacom Tanzania kwa kuongoza katika ubunifu wa huduma na Teknolojia hapa nchini.

Amesema teknolojia hii itakuwa na manufaa katika sekta zote za uchumi na kijamii nchini na itasaidia kuleta maendeleo na mageuzi kwa watanzania wote na kupelekea Tanzania kuwa na uchumi wa Kidijiti. "Teknolojia hii mtambuka, itanufaisha sekta zingine kama vile: Nishati, Madini, Ujenzi wa viwanda, Kilimo, Afya, Elimu na Usafiri. Lakini pia kuongeza kasi zaidi ya huduma za serikali mtandao.

Haya yote, yakiwa ni maeneo ambayo serikali ya awamu ya sita imeyapa kipaumbele sambamba na Tanzania ya Kidijitali ambayo yote yanatiliwa mkazo na nia yetu ya kuboresha maisha ya watu wetu na kutengeneza fursa za ukuaji wa uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla" ameyazungumza Waziri Nape.

Amesema, mapema mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alithibitisha tena dhamira ya serikali ya kuendelea kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara nchini Tanzania na Serikali inathamini jukumu la sekta binafsi katika kukuza biashara na uwekezaji na itadumisha mazungumzo ya wazi ili kujenga na kuimarisha ushirikiano na makubaliano.

Amesema Serikali imekuwa ikiweka nguvu zake katika miradi na mipango kadhaa kueneza mawasiliano nchini ikiwemo upanuzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano, Mradi wa Tanzania ya Kidijiti pamoja na Mradi wa Mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi.

"Tunafurahi sana kuona makampuni binafsi ikiwemo Vodacom yakiweza kutumia fursa na rasilimali hizi katika kuziongeza thamani. Teknolijia hii ya 5G ni njia moja itakayoongeza ufanisi wa Mkongo wa Taifa wa mawasiliano kwa kuwezesha watumiaji wake kufikia kasi ambazo ni mojawapo ya malengo makuu ya serikali katika uwekezaji mkubwa katika mkongo huo, uzinduzi huu ni sehemu ya kutimiza ndoto zetu", amesema.

Kwa upande wake Mkuu wa Mawasilino na Teknolojia wa Kampuni ya Vodacom amesema, katika kuhakikisha maendeleo ya kidijitali nchini Tanzania, watahakikisha mpaka kufikia mwaka 2024, watafikia asimia 90 ya Watanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




# BARAZA LA MAWAZIRI LIMERIDHIA UTUNGWAJI WA SHERIA YA ULINZI WA TAARIFA BINAFSI

Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mh. Nape Nauye (Mb) amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Habari, itahakikisha inaweka nguvu kubwa ili kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha uchumi wa kidijitali Afrika Mashariki kufuatia uwekezaji mkubwa unaofanywa kupitia sera na mipango mbalimbali ya kimaendeleo.

Waziri Nape ameyasema hayo Septemba 7, 2022 katika kongamano la siku mbili la kuunganisha wadau wa TEHAMA na Miundombinu (Connect 2 Connect) ndani na nje ya Tanzania katika ukumbi wa mikutano Serena Hotel jijini Dar es Salaam na kusema kuwa, serikali itamuunganisha kila mwananchi kutumia baraka ya Teknolojia ya Mawasiliano na kubadilisha maisha ya mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

“Uwepo wenu hapa unaiweka Tanzania kwenye ramani nzuri kwa kuonesha hatupo tayari kumuacha hata mtu mmoja nyuma, lakini kwa niaba ya Serikali niwahakikishie kuwa tutamuunganisha kila mmoja kutumia baraka ya teknolojia na mendeleo yake, na Baraza la Mawaziri limeruhusu kutungwa sheria itakayolinda taarifa binafsi na tunataka anga la mtandao wa Tanzania liwe salama kwa kutunga sheria bora” amesema.

Amesema Serikali imepokea maoni ya wananchi na wadau wote waliopendekeza mabadiliko katika sekta ya mawasiliano nchini na hivyo kwenda kusomwa

Amesema, ili kuhakikisha matumizi mazuri ya mtandao na teknolojia, serikali itahakikisha maadili ya utumiaji wa mtandao ili kulinda kizazi cha sasa na kijacho kwa kufikisha elimu kwa vijana kutumia fursa mbalimbli zilizopo mitandaoni kujiinua kiuchumi, na kuwakaribisha wadau mbalimbali kuweka nguvu zaidi katika ukuaji wa teknolojia na mawasiliano nchini.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni binafsi inayojenga minara na inayofanyakazi na kampuni zote za mawasiliano nchini Helios Tower Tanzania (HTI) Bwn Gwakisa Stadi amesema HTT imedhamiria kuwa mstari wa mbele katika urahisishaji na ukuaji wa mawasiliano simu barani Afrika na Mashariki ya Kati, ikitambua umuhimu mkubwa wa uungwanishwaji Pamoja na manufaa yake kwa Watanzania na HTT inajivunia kuwa mmoja wa mfadhili wa Conect 2 Connect Summit.

Kwa upande wake Bwan Tariq H Malik, Mkurugenzi wa kampuni ya Extensia Tanzania amesema kutokana na umuhimu wa Mawasiliano na Teknolojia katika Nyanja mbalimbali za kimaendeleo kama biashara, elimu, sayansi na afya, watahakikisha wanashirikiana na serikali kuwa na miundombinu rafiki kwa ajili ya kizazi kijacho, na kuwapongeza wadau mbalimbali wa sekta ya mawasiliano ikiwemo TTCL kwa kufikisha mawasiliano Mlima Kilimanjaro pamoja na kampuni ya Vodacom kwa kuwa kampuni ya kwanza Tanzania kuleta huduma Yenye kasi ya 5G na kupitia mifano hiyo, sekta ya mawasiliano nchini inakua kwa kasi zaidi.




# C2C KUCHANGIA UKUWAJI WA SEKTA YA MAWASILIANO NA UTALII ZANZIBAR

Waziri wa Miundombinu, Mawasiliano na Uchukuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dkt. Khalid Salum Mohammed (Mb) amesema kongamano la kuunganisha wadau wa TEHAMA na Miundombinu (Connect 2 Connect Summit) lina mchango mkubwa katika ukuaji wa huduma za mawasiliano nchini kutokana na mchango wa kifikra na mawazo yaliyopatikana kwa siku zote mbili.


Waziri Khalid ameyasema hayo wakati akifunga kongamano hilo Septemba 8, 2022 na kueleza kuwa, Tanzania imepata wigo mkubwa wa kujua hatua zilizofikiwa na kila mmoja katika sekta ya mawasiliano ya kidigitali na kupata mbinu mbalimbali zitakazo saidia kukua kwa mawasiliano katika uchumi, afya na sekta zote nchini Tanzania na kuendana na kasi ya uchumi wa kidigitali.

“Sasa hivi tumeingia katika ulimwengu wa kidigitali na kila kitu kinakwenda katika hali hiyo na kasi sana na uchumi wetu pia tumeuegemeza huko na ukuaji wa huduma za mawasiliano tumewekeza huko, kwahiyo ni lazima na ni muhimu na sisi kama jamii katika dunia, kuwa sambamba na wenzetu wa digital age” amesema.

Amesema katika kuhakikisha Tanzania ina imarika katika ulimwengu wa kidigitali, mwaka kesho kongamano hilo litafanyika upande wa Zanzibar kutokana na uwepo wa miundombinu rafiki inayowezesha Watanzania kunufaika kimawasiliano.

“Nchi yetu ipo tayari kwa kuwa na miundombinu ya kimawasiliano na yote ni kutokana na jitihada kubwa zilizofanywa na Serikali zetu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweka kipaumbele ajenda ya maendeleo ya nchi yetu. Wao wamevutika na jitihada za serikali zetu zote mbili na mwakani tumeamua kufanya kwa upande wa Zanzibar” amesema.

Sambamba na hilo Waziri Khalid amefafanua kuwa, huduma za mawasiliano zimefikishwa nchi nzima katika mikoa na wilaya, ambapo zaidi ya asilimia 60 Tanzania bara, zimefikiwa na mkongo wa mawasiliano na upande wa Zanzibar wilaya zote 11 zimefikiwa pia.





# MHE. MHA. KUNDO: TANZANIA KUWA KITOVU CHA TEHAMA

Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano Na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mha. Kundo Mathew (Mb) amewataka Watumishi wa Wizara hiyo kupanga mipango na mikakati ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zake ili kuhakikisha inaboresha mifumo ya TEHAMA na kuendelea kurahisisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Amesema hayo wakati wa kikao cha tathmini ya utendaji kwa Menejimenti ya Wizara na Taasisi zake kilichofanyika tarehe 26, Julai 2022 katika ukumbi wa Kibo Palace, jijini Arusha

Vilevile Mhe. Mha. Kundo ameongeza kuwa ili kuendana na mabadiliko ya TEHAMA yanayoendelea duniani ni lazima Serikali kupitia Wizara hiyo ifanye tathimini nzuri ya kujua yanayopaswa kufanyika ili kuboresha miundombinu ya TEHAMA.

“Ili tuhakikishe kwamba Tanzania inakuwa kituo cha ICT HUB ni lazima mipango hii ikakamilishwe kwa weledi kwa sababu ili uende mbele ni lazima ufanye tathmini ya tunakotoka, tulipo, na hata tunapoelekea”.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Jim Yonazi amesema kuwa umuhimu wa mkutano huo ni kuainisha mipango, kuleta utofauti katika utendaji kazi, kutoa dira mpya na kutekeleza sera mbalimbali ya Wizara vilevile kuibua fursa mpya zilizopo katika Wizara na kuleta ushindani wa kiuchumi dhidi ya nchi nyingine

Katika hatua nyingine akizungumza kwa njia ya simu Waziri wa Habari, Mawasiliano Na Teknolojia Ya Habari Mhe. Nape Nnauye amesisitiza umoja kuwa msingi katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo Pamoja na Taasisi zake.





# NAIBU WAZIRI KUNDO ARIDHISHWA NA UJENZI WA OFISI YA WIZARA

Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Mhandisi Kundo Mathewameridhishwa na maendeleo ya ujenzi wa jengo la Ofisi ya Wizara hiyo unaoendelea kufanyika alipotembelea na kukagua ujenzi huo Agosti 26, 2022 katika mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

Mhandisi Kundo amepongeza timu nzima ya wataalamu wa kandarasi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) kwa kufanya kazi kwa weledi, kujitoa pamoja na ubunifu utakaorahisisha ujenzi kumalizika mapema kabla ya muda wa mkataba.

"Mradi huu wa ujenzi wa ofisi ya Wizara umefikia asilimia 43 ikiwa ni miezi 10 tangu mradi huu uanze kutekelezwa na unatarajiwa kumalizika ndani ya miezi sita kuanzia sasa kama mkandarasi alivyoahidi", amesema Mhandisi Kundo

Ameongeza kuwa ujenzi wa jengo hilo umezalisha ajira za muda mfupi zaidi ya 160 kwa watanzania ikiwa ni moja ya manufaa ya ujenzi wa ofisi mbalimbali za Serikali zinazoendelea kujengwa katika mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma.

" Tunaishukuru Serikali ya Rais Samia kwa kufanikisha ujenzi wa ofisi za serikali ambao pamoja na mambo mengine zimezalisha ajira za muda mfupi kwa wananchi na kuwaingizia kipato kwa ajili ya mahitaji yao na familia zao", amezungumza Naibu Waziri huyo.

Aidha, Mhandisi Kundo amewataka kuwa makini katika ukamilishaji kazi hiyo na kuwakumbusha asilimia zilizobaki ni nyingi na kuwaomba wazingatie muda na ubora katika kukamilisha jengo hilo.

Naye Mkurugenzi wa Manunuzi na Ugavi wa Wizara hiyo Armon MacAchayo amelitaka Shirika la Nyumba la Taifa kuongeza kasi zaidi bila kuathiri ubora na viwango vya ujenzi wa jengo hilo ili kumaliza ujenzi kabla ya muda wa mkataba.

Ujenzi wa jengo la ofisi ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari unatarajiwa kugharimu zaidi ya billion 23 ambapo hadi sasa kiasi cha shilingi billion 8 sawa na asilimia 23 ya malipo ya jengo nzima zimekwishatumika.

Amesema kuwa katika ujenzi wa jengo hilo kumezalishwa ajira zaidi ya 160 kwa watanzania ambao wanafanya kazi eneo hilo na kumshukuru Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan katika uzalishaji wa ajira kwa familia za watanzania wanaofanya kazi katika mji huo wa mtumba na kuwataka watanzania wawe wazalendo.



# WATENDAJI SEKTA YA UMMA NA BINAFSI WATAKIWA KUSHIRIKIANA KUIJENGA TANZANIA YA KIDIJITI

Watendaji wa taasisi za umma na binafsi ambao wanatekeleza ajenda ya kuipeleka nchi katika uchumi wa kidijiti wametakiwa kushirikiana na kutekeleza jukumu hilo kwa weledi na ubora wa viwango vya Kimataifa.

Akizungumza katika Jukwaa la Nne la Ubunifu na Teknolojia lililofanyika jijini Dar es Salaam Agosti 19, 2022 Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi amesititiza ushirikishaji baina ya sekta ya umma na binafsi ili kutimiza malengo ya kuwa na Tanzania ya Kidijiti tunayoihitaji kwa maendeleo ya Taifa.

Amesema kuwa, kuna fursa nyingi za kiuchumi katika ulimwengu wa kidijiti na Wizara hiyo ipo tayari kupokea na kufanyia kazi maoni ya wadau wa sekta ya umma na binafsi kuhusu nini kinahitaji maboresho katika kufikia dira na malengo ya Taifa ya kuijenga Tanzania ya Kidijiti.

Dkt. Yonazi amezungumzia juhudi kubwa inayofanywa na Serikali ya kuongeza matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) inayoendesha uchumi wa kidijiti kwa kuongeza wigo wa usambazaji wa miundombinu na ufikishaji wa huduma za TEHAMA nchini.

"Kama mnavyofahamu hivi karibuni kupitia Shirika letu la Mawasiliano la TTCL tumefikisha intaneti yenye kasi katika Mlima Kilimanjaro na mradi wa kufikisha intaneti majumbani "fiber to home" tayari umeanza kutekelezwa na TTCL lengo ni kufikia uchumi wa kisasa wa kidijiti katika nchi yetu", amesema Dkt. Yonazi

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), Dkt. Amos Nungu amesema kuwa Jukwaa la Ubunifu na Teknolojia limewakutanisha wataalamu wabobezi, watafiti, wabunifu na watunga sera ili kujadili na kutoka na taswira tofauti ya kuijenga Tanzania ya Kidijiti kwa kuangazia vipaumbele na mahitaji ya watanzania.

Jukwaa hilo la Nne la Ubunifu na Teknolojia lilikuwa na kauli mbiu ya Tanzania ya Kidijitali Tunayoihitaji, Hatua zipi zichukuliwe Kuifikia? liliandaliwa na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Mpango wa Maendeleo (UNDP) kupitia programu ya ubunifu ya FUNGUO na kuwakutanisha wadau wa Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kutoka taasisi za umma na binafsi.



# WAFANYAKAZI WA POSTA WATAKIWA KUWA NA UBUNIFU WENYE TIJA

Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi amewataka wafanyakazi wa Shirika la Posta Tanzania kuwa na ubunifu utakaoleta tija kwenye Shirika na Taifa kwa ujumla.

Ameyasema hayo leo tarehe 19 Agosti, 2022 wakati wa hafla ya kuwapongeza viongozi pamoja na wafanyakazi hodari wa Shirika la Posta katika Makao Makuu ya Shirika hilo, jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo Dkt. Yonazi amesema, bidii na ubunifu ndiyo njia pekee itakayoliwezesha Shirika kufika mbali zaidi kiutendaji na ndiyo kupelekea kuongezeka kwa mapato ya Shirika yatakayoleta tija kwa Taifa

Aidha, Katibu Mkuu amewapongeza viongozi na wafanyakazi hodari wa Shirika hilo kwani juhudi na bidii ndiyo iliyowapelekea kupata nafasi hiyo. Hata hivyo, amelitaka Shirika kuwazingatia wafanyakazi wenye nafasi za chini ambao ndiyo wanaowawezesha Viongozi kuonekana kufanya vizuri katika utendaji wao

Vilevile, Dkt. Yonazi ametumia hafla hiyo kulipongeza Shirika la Posta kwa jitihada zake mbalimbali za kuendelea kuboresha huduma zake ili kuendana na maendeleo ya Teknolojia Pamoja na mahitaji ya wananchi.

Sambamba na hilo Katibu Mkuu Dkt. Yonazi ametoa malekezo kwa Shirika kuhakikisha linaweka kigezo cha Ubunifu wa Biashara Mpakani (Cross Border Business) kwa Viongozi na wafanyakazi ili kuwahamasisha wafanyakazi wa Posta kuongeza bidii katika kutafuta fursa za kibiashara mpakani mwa Tanzania.

Naye kwa upande wake Postamasta Mkuu wa Shirika la Posta Tanzania Ndg. Macrice Mbodo amemshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Jim Yonazi kwa kufika katika hafla hiyo na kuahidi Shirika litaendelea kuongeza bidii katika utendaji wake ili kuendelea kuwapatia wananchi huduma bora na zinazoendana na mahitaji yao.





## KITUO CHA 2 AFRIKA KUWA KITOVU CHA MAWASILIANO AFRIKA MASHARIKI

Tanzania itakuwa kitovu cha maunganisho wa mawasiliano Afrika Mashariki na Kati kufuatia uwepo wa mkongo wa mawasiliano wa 2 Afrika utakapokamilika mwakani mwezi februari.

Hayo yameelezwa na Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt Jim Yonazi alipofanya ukaguzi wa mkongo wa kituo cha 2 Afrika Septemba 9, 2022 na kueleza kuwa hilo linafanyika kutokana na juhudi za Serikali kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha maunganisho ya mawasiliano.

Amesema kukamilika kwa ujenzi wa kituo hicho unafaida kubwa kwa nchi yetu kwa kupata mtandao wa Intaneti yenye kasi zaidi na uhakika wa kuunganishwa duniani.

“Mkongo unaokuja unapitia kusini mwa bara la Afrka, kwahiyo tutapata uhakika wa maunganisho kwenda duniani na kusaidia sana biashara ya kuuza capacity nchini mwetu nan chi Jirani na kuwasaidia wananchi wetu nan chi Jirani kuweza kushiriki katika uchumi wa kidigitali ambao ndio uchumi sasa dunia inashiriki” amesema.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Kampuni ya Airtel Tanzania, Bi. Beatrice Singano amesema wanatengeneza eneo la kusambaza mawasiliano yanayopitia baharini (Sea Cable Services) ili kuiwezesha Tanzania kufikiwa na kufikia maeneo mengine kimawasiliano.

Kituo cha Mkongo wa 2Africa Submarine kinatarajiwa kukamilika mwanzoni mwa mwaka 2023 kwa kufika katika Zaidi ya maeneo 35 katika nchi 26 Duniani.



## DKT. YONAZI ATEMBELEA KIWANDA CHA SMART CARD CHA DZ CARD AFRICA LTD

Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Jim Yonazi Septemba 09, ametembelea kanda maalum ya Kiuchumi ya Benjamin William Mkapa Mabibo Jijini Dar es Salaam.

Dkt. Yonazi amekagua na kujionea kazi mbalimbali zinazofanywa na kiwanda cha kutengeneza SMART CARD cha DZ CARD AFRICA LIMITED kama anavyoonekana katika picha mbalimbali akiwa na maafisa wa Wizara hiyo alioongozana nao, Uongozi wa EPZA na kiwanda cha DZ CARD AFRICA LIMITED.

Akizungumza mara baada ya kukagua kazi za kiwanda hicho Dkt. Jim Yonazi ameahidi kutoa ushirikiano zaidi katika kukuza Teknolojia na Uwekezaji nchini kwa ujumla ili kuendeleza dhamira njema ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan ya kukuza uchumi wa Nchi na kuongeza ajira kwa



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Jim Yonazi (wakatikati) akizungumza na Mwanzilishi wa Kampuni ya Vesterbacka Finest Future na Mchezo wa Kompyuta (game) ujulikanao kama Angry Birds, Bw. Peter Vesterbacka (kulia) ofisini kwake tarehe 9 Septemba 2022, jijini Dar es Salaam. Wa kwanza kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya TEHAMA Tanzania, Dkt. Nkundwe Moses Mwasaga.*




# NAIBU KATIBU MKUU AFANYA ZIARA USCAF

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Bw. Mohammed Khamis Abdulla leo Agosti 10, 2022 ametembelea Makao Makuu ya Ofisi za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) zilizopo jijini Dodoma.

Pamoja na mambo mengine Naibu Katibu Mkuu Abdulla amefanya kikao cha pamoja na wafanyakazi wa Mfuko huo kwa lengo la kupata taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa majukumu ya Mfuko.

Aidha, Naibu Katibu Mkuu huyo akiambatana na Mtendaji Mkuu wa UCSAF, Bi. Justina Mashiba ametembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa ofisi mpya za UCSAF unaoendelea katika eneo la Njedengwa jijini Dodoma ambapo ujenzi huo umefikia asilimia 97.





## ZIARA YA KIKAZI MAENDELEO YA MRADI WA UJENZI WA MINARA 42 ZANZIBAR

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Bw. Mohammed Khamis Abdulla amefanya ziara ya kukagua minara 42 itokanayo na mradi wa Rural Telecommunication Border & Special Zone Phase 7 (BSZPH7) ilyojengwa na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) kwa kushirikiana na kampuni ya Tigo-Zantel tarehe 29 Agosti, 2022, Zanzibar.

Kupitia ziara hiyo, Bw. Mohammed Abdulla amezipongeza UCSAF na kampuni ya Tigo-Zantel kwa utekelezaji wa mradi huo kwa ufanisi mkubwa na kupelekea kupunguza tatizo kubwa la huduma za mawasiliano katika maeneo mbalimbali ya unguja vijijini.



# MFANYAKAZI HODARI KITAIFA WA WIZARA

Mhandisi Jampyon Peter Mbugi ni Mhandisi Mwandamizi wa Mawasiliano katika Idara ya Mawasiliano ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Mhandisi Mbugi amekuwa Mtumishi wa Serikali tangu mwaka 2009 na amekuwa akishiriki katika kazi mbalimbali za kiufundi za miradi ya mawasiliano, ikiwa ni pamoja na kuwa Mratibu wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mfumo wa Anwani za Makazi kuanzia 2018.

Hivi karibuni, Mhandisi Mbugi alichaguliwa kuwa Mfanyakazi Hodari wa Kitaifa wa Wizara. Katika mahojiano naye juu ya siri ya kuwa Mfanyakazi Hodari; pamoja na masuala mengine Mhandisi Mbugi amesema “kimsingi sikuwahi kufikiri kama itakuja kutokea kwa Wizara yetu kutoa Mfanyakazi Hodari Kitaifa tena mfanyakazi mwenyewe mimi, kwa sababu ni miaka zaidi ya 10 nipo hapa Wizarani sijawahi kushuhudia tukio hili”.

Ameeleza kuwa katika utendaji kazi wake anapenda shughuli yoyote anayoifanya ama kuiratibu ikamilike kwa tija, ufanisi na muda uliyopangwa; na iwe na manufaa kijamii na kiuchumi. “Nimejenga tabia ya kufanya kazi kwa kujituma ili kuhakikisha majukumu niliyopewa yana tija na mafanikio makubwa kwa Maslahi ya Taifa, nafikiri hili ndiyo chimbuko la kuwa Mfanyakazi Hodari, alisema Mhandisi Mbugi.

Mhandishi Jampyon Peter Mbugi alizaliwa tarehe 10 Januari 1978 katika kijiji cha Ikomelo, Mkoani Mbeya. Mhandisi Mbugi alihitimu elimu ya msingi katika shule ya msingi Msolwa Station. Aliendelea na elimu katika Shule ya Sekondari ya Ufundi ya Ifunda, iliyopo Iringa na baadae Chuo cha Ufundi Mbeya ambacho kwa sasa kinaitwa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya.

Aidha, Mhandisi Mbugi ana Shahada ya Uhandisi wa Mawasiliano (Bachelor Degree in Electronics and Telecommunication Engineering) ambayo aliipata katika Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph kilichopo Dar es Salaam, mwaka 2009 na Shahada ya Uzamili ya Mawasiliano katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, mwaka 2022.

# Je Wajua?



**Danieli N. Mloka** ndiye aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi mwaka 1978 - 1979. Katika kipindi hicho, Wizara yetu ilikuwa ikijulikana kama Wizara ya Mawasiliano na Ujenzi.




JARIDA LA MAWASILIANO TOLEO LA 25

Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari
S.L.P. 677, 40470 Dodoma, Tanzania
Barua pepe: ps@mawasiliano.go.tz
Tovuti: www.mawasiliano.go.tz
Instagram: Wizarahmth
Twitter: Wizarahmtm